

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
26 Aprili, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AWATAKA WATANZANIA KUDUMISHA MUUNGANO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania kuendeleza Muungano kwa kuitekeleza falsafa ya Maridhiano, Ustahmilivu, Kuleta Mageuzi na Kujenga nchi yetu (**4R**).

Aidha, Rais Samia amesema Falsafa ya **4R** ndio itakayoendelea kuijengea nchi yetu amani na utulivu wa kudumu pamoja na kuleta maendeleo endelevu.

Rais Samia amesema hayo leo wakati akihutubia katika kilele cha sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika katika uwanja wa Uhuru.

Rais Samia pia amesema Watanzania wanapaswa kujivunia Muungano kwani umetuwezesha kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa, kuimarisha udugu, kudumisha mila na desturi na kupiga hatua kubwa za maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Hivyo, Rais Samia amewataka Watanzania kuendelea kudumisha amani ili kuendelea kujenga uchumi wa nchi na kuleta ustawi zaidi wa wananchi.

Hali kadhalika, Rais Samia amewasihi Watanzania kuendelea kufanya kazi kwa bidii na maarifa zaidi ili kukuza tija kwa ustawi wa taifa na kuwezesha kupatikana kwa haki za msingi za maisha ya binadamu pamoja na kustawisha utu wa wananchi.

Kwa upande mwingine, Rais Samia ametoa pole kwa Watanzania wote walioathiriwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha na amewahakikishia kuwa Serikali inaendelea kufanya jitihada kuhakikisha inarejesha miundombinu iliyoathiriwa.

Vile vile, Rais Samia ametoa wito kwa wananchi kufuata na kuzingatia tahadhari zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kuepuka madhara.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

